# 02 - Historia Fupi Ya Makkah Na Kuhusu Hajj Na 'Umrah

## Makkah

Imeanza pale Allaah (سبحانه وتعالى) Alipomuamrisha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) ahamie huko pamoja na mkewe wa pili Haajar na mwanawe Ismaa'iyl. Wakati huo Makkah ilikuwa ni bonde tu ambalo hapakuwa na chochote wala wakazi wowote.

﴿ وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِـۧمُ رَبِّ ٱجْعَلْ هَـٰذَا بَلَدًا ءَامِنًا وَٱرْزُقْ أَهْلَهُۥ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ مَنْ ءَامَنَ مِنْهُم بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْـَٔاخِرِ ﴾

**((Na (taja) aliposema Ibraahiym: "Rabb wangu Ufanye mji huu kuwa wa amani na Waruzuku watu wake katika matunda atakayemwamini Allaah miongoni mwao na Siku ya Mwisho"))**[1]

## *Al-Ka'bah*

Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَـٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾ ﴾

**((Hakika nyumba ya awali iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya 'ibaadah) ni ile ambayo iko Bakkah (Makkah), yenye barakah na mwongozo kwa walimwengu.))**[2]

## *Twawaaf*

Nayo pia imeanza wakati huo huo wa Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) pale Allaah (سبحانه وتعالى) Anaposema:

---

[1] Al-Baqarah (2: 126).
[2] Aal-'Imraan (3: 96).

﴿ وَإِذْ جَعَلْنَا ٱلْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمْنًا وَٱتَّخِذُوا۟ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّى ۖ وَعَهِدْنَآ إِلَىٰٓ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَـٰعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْعَـٰكِفِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿١٢٥﴾ ﴾

**((Na (taja) Tulipoifanya Nyumba kuwa ni mahali pa kurejewa na watu na (mahali pa) amani, na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia. Na Tulichukua ahadi kwa Ibraahiym na Ismaa'iyl kwamba: "Itakaseni Nyumba Yangu kwa wanaotufu na wanaokaa i'tikaaf, na wanaorukuu na kusujudu"))[3]**

## *Ar-Raml*

*Ar-Raml* ni kuenda mwendo wa mbio mbio kwa hatua fupi fupi. Ni Sunnah inayotakiwa kutekelezwa katika *Twawaaful-Quduwm*. Sunnah hii haitekelezwi na wanawake wala watoto bali wanaume pekee. Ilianza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipowaamrisha Maswahaba watufu *Al-Ka'bah* kwa mwendo wa haraka katika *Twawaaf* tatu za mwanzo kwa sababu ya kudhihirisha nguvu mbele ya makafiri ili isidhaniwe kuwa hali yao bado ni dhaifu kutokana na ugonjwa waliopata kabla ya kuingia kufanya 'Umrah mara ya kwanza kabisa baada ya Hijrah:

عن ابن عباس (رضي الله عنهما) قال : "قدم رسول الله صلى الله عليه وسلم وَأَصْحَابِهَ، فَقالَ الْمُشْرِكُونَ: "إِنَّهُ يَقْدُمُ عَلَيْكُمْ قَوْمٌ قَدْ وَهَنَتْهُمْ حُمَى يَثْرِب". فَأَمَرَهُمُ النَّبِيّ (صلى الله عليه وسلم) أَنْ يَرْملوا الأَشْوَاط الثَّلاثَة (وفي رواية زيادة): قال: **((اِرْملوا ليَرى الْمُشْرِكُون قُوَّتكُمْ))**

Imetoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba alifika Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake (Makkah) washirikina wakasema: "Wamekufikieni watu ambao wamedhoofika kutokana na homa ya Yathrib". Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) akawaamrisha wafanye *Ar-Raml* mizunguko mitatu" (ya *Twawaaf*) na katika riwaaya nyingine imezidi: ***((Fanyeni Ar-Raml ili washirikina waone nguvu zenu))[4]***

[3] Al-Baqarah (2: 125).
[4] Al-Bukhaariy na Muslim.

## Fadhila za *Twawaaf*

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kwamba amemsikia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema:

((مَنْ طَافَ بِهَذَا الْبَيْتِ سُبُوعًا فَأَحْصَاهُ كَانَ كَعِتْقِ رَقَبَةٍ)) صحيح الترمذي

**((*Atakayetufu Nyumba hii, mara saba, akazihesabu barabara atapata fadhila za kuacha huru mtumwa*))**[5]

Na pia kamsikia akisema:

((لَا يَضَعُ قَدَمًا وَلَا يَرْفَعُ أُخْرَى إِلَّا حَطَّ اللَّهُ عَنْهُ خَطِيئَةً وَكَتَبَ لَهُ بِهَا حَسَنَةً))

***((Hakanyagi mtu mguu wala haunyanyui mwengine isipokuwa Allaah Humfutia dhambi na Humuandikia jema moja))***[6]

## *Rukn Al-Yamaaniy*

Imesemekana imejengwa na mtu kutoka Yemen[7]. Pia tokea 'Abdullaahi bin Zubayr (رضي الله عنه) alipojenga *Al-Ka'bah* akaiweka ikabakia hadi leo[8]. Inapendekeza kugusa tu kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) bila ya kubusu au kuleta *takbiyr*.

## Fadhila za *Rukn Al-Yamaaniy*

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

---

[5] *Swahiyh At-Tirmidhiy*.

[6] Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Umar - Sunan At-Tirmidhiy (959) na katika *Swahiyh At-Targhiyb* (1139).

[7] *Mu'jam Al-Buldaan (3/64) – Yaaquwt Al-Hamwy.*

[8] *At-Taariykh Al-Qadiym li-Makkah wa-Bayt Allaahil-Kariym* – Muhammad Twaahir Al-Kurdiy Al-Makkiy (3/256).

((إِنَّ الرُّكْنَ وَالْمَقَامَ يَاقُوتَتَانِ مِنْ يَاقُوتِ الْجَنَّةِ طَمَسَ اللَّهُ نُورَهُمَا وَلَوْ لَمْ يَطْمِسْ نُورَهُمَا لأَضَاءَتَا مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ))

***((Hakika Ar-Rukn na Al-Maqaam ni yaquti mbili katika yaquti za Jannah, Allaah Amezima mwanga wake, na lau kama Hakuzima mwanga wake, ungeliangaza yaliyoko baina ya Mashariki na Magharibi))***[9]

### *Al-Hajar Al-As-wad*

*Al-Hajar Al-As-wad* liko pembe ya Mashariki ya *Al-Ka'bah* kutoka *Rukn Al-Yamaaniy* ambayo iko Kusini Mashariki mwa *Al-Ka'bah*. Ni jiwe tukufu kabisa duniani na pia ni tukufu kabisa katika *Al-Ka'bah* Jiwe ni kubwa mno ila limeingizwa ndani zaidi ya *Al-Ka'bah* hivyo sehemu inayoonekana ni sehemu ndogo kabisa kulingana na iliyoingizwa ndani. *Al-Hajar Al-As-wad* limeteremshwa kutoka Jannah akalipokea Ismaa'iyl kutoka kwa Jibriyl kumalizia kujenga *Al-Ka'bah*.

*Al-Hajar Al-As-wad* ni alama ya pahali pa kuanzia na kumalizia *Twawaaf* na linabusiwa panapokuwa na uwezekano.

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) akisema: "Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alifanya *Ar-Raml* kuanzia *Al-Hajar Al-As-wad* (jiwe) mpaka *Al-Hajar Al-As-wad* mara tatu kisha akatembea (kikawaida katika kutufu *Al-Ka'bah*) mara nne"[10]

Pia imetoka kwa Jaabir bin 'Abdullaah (رضي الله عنه) kwamba: "Tulitoka pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) katika *Hajjat Al-Widaa'* hadi tulipofika katika Nyumba (*Al-Ka'bah*) alilibusu *Al-Hajar Al-As-wad* kisha akatufu mizunguko mitatu kwa *Ar-Raml* na (*Twawaaf*) nne kwa mwendo wa kawaida"[11]

### Fadhila Za *Al-Hajar Al-As-wad*

---

[9] Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Amru - *Swahiyh At-Tirmidhiy* (878), Ibn Khuzaymah (4/220), Ahmad (1/207-229-373).

[10] Muslim katika Kitaab *Al-Hajj* (2213).

[11] Muslim 1218.

**((الْحَجَرُ الْأَسْوَدُ مِنْ الْجَنَّةِ))**

***((Al-Hajar Al-As-wad linatoka Jannah))***[12]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ (رضي الله عنهما) قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ **((نَزَلَ الْحَجَرُ الْأَسْوَدُ مِنْ الْجَنَّةِ وَهُوَ أَشَدُّ بَيَاضًا مِنْ اللَّبَنِ فَسَوَّدَتْهُ خَطَايَا بَنِي آدَمَ))**

Imepokelewa toka kwa ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Al-Hajar Al-As-wad limeteremka kutoka Jannah likiwa jeupe kuliko maziwa, likasawijika (kuwa jeusi) kwa dhambi za bin Aadam))***[13]

عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الْحَجَرِ: **((وَاللَّهِ لَيَبْعَثَنَّهُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَهُ عَيْنَانِ يُبْصِرُ بِهِمَا وَلِسَانٌ يَنْطِقُ بِهِ يَشْهَدُ عَلَى مَنْ اسْتَلَمَهُ بِحَقٍّ))**

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Naapa kwa Allaah! Allaah Atalileta Siku ya Qiyaamah likiwa na macho mawili ambayo litaweza kuona na ulimi utakaosema, na litashuhudia kwa kila aliyeligusa kwa haki))***[14]

**((إِنَّ مَسْحَ الْحَجَرِ الأَسْوَدِ ، والركنَ اليمانيّ، يَحُطَّانِ الخطايا حطًّا))**

***((Kugusa Al-Hajar Al-As-wad na Ar-Rukn al-Yamaaniy ni kufutiwa madhambi))***[15]

### *Maqaam Ibraahiym*

Ni mahali aliposimama Ibraahiym (عليه السلام) kumalizia kujenga kuta za juu za *Al-Ka'bah*. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

---

[12] Hadiyth ya Anas katika *Swahiyh Al-Jaami'* (3175).
[13] Ibn Maajah katika *Swahiyh Al-Jaami'* (6756), *Swahiyh At-Tirmidhiy* (877).
[14] *Swahiyh At-Tirmidhiy* (961), Ibn Maajah (2944).
[15] Hadiyth ya Ibn 'Umar katika *Swahiyh Al-Jaami'* (2194).

﴿ إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَـٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾ فِيهِ ءَايَـٰتٌۢ بَيِّنَـٰتٌ مَّقَامُ إِبْرَٰهِيمَ ﴾

**((Hakika nyumba ya awali iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya 'ibaadah) ni ile ambayo iko Bakkah (Makkah), yenye barakah na mwongozo kwa walimwengu. Ndani yake kuna *Aayaat* (ishara, dalili) zilizo wazi; mahali pa kisimamo cha Ibraahiym.))**[16]

Inasemekana pia ni mahali aliposimama Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kuwatangazia watu kuja kutekeleza 'Ibaadah ya Hajj.

Mahujaji wanapomaliza kutufu *Al-Ka'bah* wanatakiwa waende hapo na kuswali rakaa mbili:

﴿ وَٱتَّخِذُواْ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّى ﴾

**((Na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia))**[17]

***Hijr***

Inadhaniwa na wengi kuwa ni *'Hijr Ismaa'iyl'* (chumba cha Ismaa'iyl) na kwamba ni chumba alichozikiwa pamoja na mama yake Haajar ndio maana pakaitwa hivyo. Hakuna uthibitisho wa hilo, na si kweli kwa sababu ingelikuwa ni hivyo mahali hapo pasingelifaa kuswaliwa kwani haifai kuswalia mbele ya kaburi. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) ameitambulisha sehemu hiyo kuwa ni 'Hijr' pekee. Sehemu hiyo imetajwa katika usimulizi ufuatao pale *Al-Ka'bah* lilipoharibiwa na kujengwa tena:

عَنْ عَائِشَةَ قَالَتْ: سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ الْجَدْرِ: أَمِنْ الْبَيْتِ هُوَ؟ قَالَ: ((**نَعَمْ**)) قُلْتُ: فَلِمَ لَمْ يُدْخِلُوهُ فِي الْبَيْتِ؟ قَالَ: ((**إِنَّ قَوْمَكِ قَصَّرَتْ بِهِمْ النَّفَقَةُ**)) قُلْتُ: فَمَا شَأْنُ بَابِهِ مُرْتَفِعًا؟

[16] Aal-'Imraan (3: 96-97).
[17] Al-Baqarah (2: 125).

قَالَ: ((فَعَلَ ذَلِكِ قَوْمُكِ لِيُدْخِلُوا مَنْ شَاءُوا وَيَمْنَعُوا مَنْ شَاءُوا, وَلَوْلَا أَنَّ قَوْمَكِ حَدِيثٌ عَهْدُهُمْ فِي الْجَاهِلِيَّةِ, فَأَخَافُ أَنْ تُنْكِرَ قُلُوبُهُمْ, لَنَظَرْتُ أَنْ أُدْخِلَ الْجَدْرَ فِي الْبَيْتِ وَأَنْ أُلْزِقَ بَابَهُ بِالْأَرْضِ))

Imetoka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) amesema: "Nilimuuliza Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kuhusu ukuta (upande wa Hijr). Je huo ni sehemu ya Nyumba (yaani *Al-Ka'bah*?)" Akajibu: ***((Ndio***)) Nikasema: "Kwa nini basi usiingizwe ndani ya Nyumba?" Akajibu: ***((Watu wako walipungukiwa na uwezo wa fedha))***. Nikasema: "Kwa nini basi mlango wake umeinuka juu?" Akajibu: ***((Watu wako wamefanya hivyo ili wamuingize wamtakaye na wamzuie wamtakae. Na ingelikuwa watu wako si waliotoka kubadili Dini na si khofu kuwa itawachukiza nyoyo zao, ningeliungiza ukuta ndani ya Nyumba na ningeliuteremsha mlango wake usawa na ardhi))***[18]

## Maji ya Zamzam, *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*

Historia yake imeanza pale Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipomwacha Makkah mkewe wa pili Haajar na mwanawe Ismaa'iyl akiwa ni mtoto mchanga wa kunyonya. Wakati huo Makkah kulikuwa hakuna chochote. Imepokelewa toka kwa ibn 'Abbaas kama ifuatavyo:

"Ibraahiym (عليه السلام) alikuja na Haajar na mwanawe Ismaa'iyl akiwa anamnyonyesha mpaka alipowasili Makkah penye bonde baina ya *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah* mahali kilipo kisima cha maji ya Zamzam hivi sasa, na wakati huo nyumba ya Allaah (سبحانه وتعالى) (*Al-Ka'bah*) ilikuwa ni sehemu iliyonyanyuka tu juu ya ardhi, ikishambuliwa na upepo mkali pamoja na mikondo ya maji ya mvua iliyokuwa ikizikwanguwa pembe nne za nyumba hiyo. Hapakuwa na mtu anayeishi mahali hapo wala nyumba wala maji isipokuwa mti mmoja alipowaacha mkewe na mwanawe chini yake, akawawekea birika la maji pamoja na chombo alichowatilia tende ndani yake, kisha akageuka na kuianza safari ndefu ya kurudi Shaam.

Mama yake Ismaa'iyl alipomuona mumewe akirudi na kuwaacha mahali hapo walipopafikia baada ya safari ndefu iliyowachukuwa siku nyingi njiani, mahali pasipo na mji wala kijiji. Hapakuwa na hata dalili ya kuwepo mtu mahali popote karibu na hapo, akamfuata mumewe na kumuuliza:

[18] Muslim 1333.

“Unatuachia nani mahali hapa pasipo na mtu yeyote?” Akamuuliza hivyo mara nyingi lakini Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) hakumjibu.

Mwisho Mama yake Ismaa’iyl akamuuliza: “Allaah Ndiye Aliyekuamrisha?” Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) akamjibu: “Naam, ndiyo.”

Kwa iymaan iliyothibiti, kwa utiifu mkubwa na kwa moyo uliosalimu amri, Bibi Haajar akamwambia: “Kwa hivyo Hatotupoteza”.

Hapo ndipo Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipogeuka na kuianza safari ndefu ya kurudi Palestina (Shaam) akimuacha nyuma mkewe na mwanawe wa mwanzo na wa pekee wakati ule, na baada ya kutembea muda kidogo mahali ambapo mkewe hakuweza kumuona, Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) akageuka nyuma na kuomba du’aa ifuatayo:

﴿ رَّبَّنَآ إِنِّيٓ أَسۡكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيۡرِ ذِي زَرۡعٍ عِندَ بَيۡتِكَ ٱلۡمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱجۡعَلۡ أَفۡـِٔدَةً مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهۡوِيٓ إِلَيۡهِمۡ وَٱرۡزُقۡهُم مِّنَ ٱلثَّمَرَٰتِ لَعَلَّهُمۡ يَشۡكُرُونَ ﴿٣٧﴾ ﴾

**((“*Rabb* wetu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuria wangu katika bonde (la Makkah) lisilokuwa na mmea wowote, kwenye Nyumba Yako Tukufu. Rabb wetu, ili wasimamishe Swalaah na Ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao na Uwaruzuku mazao ili wapate kushukuru))**[19]

Bibi Haajar akawa anakula zile tende alizowekewa na mumewe huku akimnyonyesha mwanawe, lakini haukupita muda mrefu maji yakaanza kupunguwa na hatimaye kumalizika, na mwanawe alipoanza kuona kiu, Bibi Haajar akaanza kuhangaika huku na kule akimtafutia maji. Akaliendea jabali lililokuwa karibu yake. ‘*Jabal Asw-Swafaa’* na kulipanda, na alipofika kileleni akaanza kutizama huku na kule akitafuta maji au msafara wa watu watakaokuwa na maji, lakini hakuona kitu. Akateremka na kuanza kutembea taratibu penye bonde lililopo baina ya jabali *Asw-Swafaa* na jabali *Al-Mar-wah*, na alipofika kati kati ya bonde akaanza kukazana huku akiliendea jabali *Al-Mar-wah* na kulipanda, na alipofika kileleni akaanza kutizama huku na kule, lakini bila mafanikio yoyote.

Anasema Ibn ‘Abbaas kuwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hiyo ndiyo As-Sa’-y mnayotembea baina ya Asw-Swafaa na Al-Mar-wah)).***

---

[19] Ibraahiym (14: 37).

Bibi Haajar aliendelea kufanya hivyo mara saba, na alipokuwa akiliendea jabali *Al-Mar-wah* akasikia sauti ngeni ikimsemesha. Alinyamaza kimya ili aisikie vizuri huku akitazama mahali alipo mwanawe, akamuona Malaika amesimama mahali kilipo kisima cha Zamzam hivi sasa, huku akichimba kwa ubawa wake mpaka maji yalipofurika, ndipo mamake Ismaa'iyl alipoyaendea na kuanza kuyachota kwa mikono yake huku akimnywesha mwanawe na kunywa yeye mwenyewe. Alipokuwa akinywa na kumnywesha mwanawe, Malaika akamwambia: "Usiogope, hutopotea, kwani hapa ndipo ilipo nyumba ya Allaah itakayojengwa na mtoto huyu na baba yake."[20]

## *Minaa*

*Minaa* iko kilo mita tano kutoka Makkah. Ni mahali ambako shaytwaan alimfuata Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kumshawishi asitekeleze ndoto yake ya kumchinja mwanawe Ismaa'iyl. Alimfuata mahali patatu; *Jamaraat Al-Kubraa*, *Al-Wuswtwaa* na *Asw-Swughraa*.

Mahujaji huanzia taratibu zao za Hajj *Minaa* wanapokuja kutoka Makkah tarehe 8 Dhul-Hijja wakiwa wameingia katika Ihraam. Makazi yao kwa wakati huo ni katika mahema na hubakia hapo hadi tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah ili wapate kumalizia 'Ibaadah za kurusha vijiwe katika minara ya *Jamaraat*. Tarehe 9 Dhul-Hijjah Alfajiri huelekea *'Arafah*, halafu huelekea *Muzdalifah*, baadae hurudi *Minaa* na kubakia hapo mpaka Wanapomaliza kurusha vijiwe ambayo huwa ni tarehe 12 au 13 Dhul-Hijjah hurudi tena Makkah na kubakia hapo au kufanya *Twawaaf Al-Wadaa'i*.

Wanapobakia *Minaa* wanapaswa kumdhukuru sana Allaah (سبحانه وتعالى)[21]

## *'Arafah*

Inasemekana kuwa ni mahali ambapo Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alisimama pia kuwatangazia watu kuja kuhiji kama alivyoamrishwa na Allaah (سبحانه وتعالى). Alipofika alisema: **عَرَفْتُ** (nimepajua).

---

[20] Al-Bukhaariy.
[21] Al-Baqarah (2: 203).

Jabali la '*Arafah* ndipo wanaposimama Mahujaji na ndio kilele cha 'Ibaadah hii tukufu kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((الْحَجُّ عَرَفَةٌ))**

**((Hajj ni '*Arafah*))**[22]

Jina la '*Arafah* limetajwa pia katika Aayah[23]

Imesimuliwa toka kwa Yaziyd bin Shaybaan kwamba: "Tulikuwa tumesimama '*Arafah* mahali mbali na *mawqif* (sehemu aliyosimama Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم). Ibn Mirba' Al-Answaariy akaja kutuambia: "Mimi ni mjumbe wa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amenituma nikuambieni: ***((Simameni mlipo (kwani hapo pia ni mahali pa wuquwf) kwani hapo ndipo mahali aliposimama baba yenu Ibraahiym (عليه السلام)))***[24]

Jabali hilo alisimama Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwakhutubia Maswahaba katika *Hajjatul-Wadaa'i* yake ambayo alitoa khutbah yenye nasaha kadhaa na mwishowe kuwataka Maswahaba wafikishe ujumbe kwa kila aliyekuwa hakufika siku hiyo na kuendeleza kizazi baada ya kizazi.

**Fadhila Za Siku ya '*Arafah***

Siku hii ni tukufu mno na fadhila zake zimetajwa katika Hadiyth kadhaa kama ifuatavyo:

- Siku iliyokamilika Dini yetu:

عَنْ طَارِقِ بْنِ شِهَابٍ قَالَ: قَالَ رَجُلٌ مِنْ الْيَهُودِ لِعُمَرَ: يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ لَوْ أَنَّ عَلَيْنَا نَزَلَتْ هَذِهِ الْآيَةُ: ﴿ ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا ۚ ﴾ لَاتَّخَذْنَا

---

[22] At-Tirmidhiy 2975).

[23] Tazama chini ya *Muzdalifah* (Al-Baqarah 2: 198).

[24] Abu Daawuwd na At-Tirmidhiy na imerekodiwa katika *Swahiyh Abi Daawuwd* (1688) ya Al-Albaaniy.

ذَلِكَ الْيَوْمَ عِيدًا. فَقَالَ عُمَرُ: إِنِّي لَأَعْلَمُ أَيَّ يَوْمٍ نَزَلَتْ هَذِهِ الْآيَةُ, نَزَلَتْ يَوْمَ عَرَفَةَ فِي يَوْمِ جُمُعَةٍ.

Imepokelewa kutoka kwa Twaariq bin Shihaab (رضي الله عنه) amesema: Myahudi mmoja alimwambia: 'Umar: "Ewe Amiyr wa Waumini, lau ingeliteremka kwetu sisi Aayah hii **((Leo Nimekukamilishieni Dini (yenu), na Nimekutimizieni neema Yangu, na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe (ndio) Dini yenu))**[25], tungeliifanya 'Iyd siku hiyo. Akasema 'Umar: "Hakika naijua siku gani imeteremka Aayah hii. Imeteremka Siku ya *'Arafah* siku ya Ijumaa"[26]
Na kukamilika Dini yao ni kukamilisha nguzo zote za Kiislamu.

- Siku Ambayo Allaah Amechukua fungamano (ahadi) kutoka kizazi cha Aadam.

Imesimuliwa kwamba Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Allaah Amechukua fungamano kutoka mgongo wa Aadam katika Na'maan yaani 'Arafah. Akatoa mgongoni mwake kizazi chake chote na Akawatandaza mbele Yake. Kisha Akawakabili kuwauliza*:**

أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوا۟ بَلَىٰ ۛ شَهِدْنَآ ۛ أَن تَقُولُوا۟ يَوْمَ ٱلْقِيَـٰمَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَـٰذَا غَـٰفِلِينَ ﴿١٧٢﴾ أَوْ تَقُولُوٓا۟ إِنَّمَآ أَشْرَكَ ءَابَآؤُنَا مِن قَبْلُ وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِّنۢ بَعْدِهِمْ ۖ أَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ ٱلْمُبْطِلُونَ ﴿١٧٣﴾

**(("Je, Mimi siye Rabb wenu?" Wakasema: "Ndiye, tunashuhudia!" (Allaah Akawaambia): "Msije kusema Siku ya Qiyaamah (kwamba) hakika sisi tulikuwa tumeghafilika nayo haya. Au mkasema: Hakika baba zetu ndio walioshirikisha kabla, nasi tulikuwa kizazi baada yao. Basi Utatuangamiza kwa yale waliyoyafanya wabatilifu"[27]**)) Hadiyth[28]

- Siku Ambayo Allaah Ameiapia

[25] Al-Maaidah (5: 3).
[26] Al-Bukhaariy.
[27] Al-A'raaf (7: 172-173).
[28] Imesimuliwa na Ahmad ameisahihisha Al-Albaaniy.

﴿ وَٱلسَّمَآءِ ذَاتِ ٱلْبُرُوجِ ۝١ وَٱلْيَوْمِ ٱلْمَوْعُودِ ۝٢ وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ ۝٣ ﴾

**((Naapa kwa mbingu zenye buruji. Na siku iliyoahidiwa (Qiyaamah). Na shahidi na kinachoshuhudiwa))**[29] Imepokelewa toka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) amesema: "Siku ya kuahidiwa ni siku ya kufufuliwa. Siku ya kushuhudiwa ni siku ya *'Arafah*, na Siku ya kinachoshuhudiwa ni Siku ya Ijumaa*))*[30].

- Ni Siku Bora Kabisa Ambayo Wataokolewa Waja Kutokana Na Moto.

عَنْ عَائِشَةُ (رضي الله عنها) إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**مَا مِنْ يَوْمٍ أَكْثَرَ مِنْ أَنْ يُعْتِقَ اللَّهُ فِيهِ عَبْدًا مِنْ النَّارِ مِنْ يَوْمِ عَرَفَةَ وَإِنَّهُ لَيَدْنُو ثُمَّ يُبَاهِي بِهِمْ الْمَلَائِكَةَ فَيَقُولُ مَا أَرَادَ هَؤُلَاءِ**)) وفي رواية: ((**اشْهَدُوا أَنِّي قَدْ غَفَرْتُ لَهُمْ**))

Imepokelewa toka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) kuwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna siku Anayoacha Allaah huru waja kwa wingi kutokana na moto kama siku ya 'Arafah. Na huwa karibu kisha Anajigamba kwao kwa Malaika na Husema: Wametaka nini hawa?))***[31] Na katika riwaayah nyingine ***((Shuhudieni Malaika wangu kwamba hakika Nimewaghufuria))***[32]

- Siku Ya Kutakabaliwa Du'aa:

Imepokelewa toka kwa babu yake 'Amru bin Shu'ayb (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((خَيْرُ الدُّعَاءِ دُعَاءُ يَوْمِ عَرَفَةَ, وَخَيْرُ مَا قُلْتُ أَنَا وَالنَّبِيُّونَ مِنْ قَبْلِي: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ))**

***((Du'aa bora kabisa ni du'aa katika siku ya 'Arafah, na yaliyo bora kabisa niliyosema mimi na Mitume kabla yangu ni: 'Laa Ilaaha Illa Allaah Wahdahu laa shariyka Lahu, Lahul-Mulku wa-Lahul-hamdu wa***

29 Al-Buruwj (85: 1-3).
30 At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Albaaniy.
31 Muslim.
32 Swahiyh At-Targhiyb ya Al-Albaaniy (1154).

***Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr – Hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah Peke Yake, Hana mshirika. Yeye Ndiye Mwenye Ufalme na Ndiye Mwenye kuhimidiwa, Naye ni Muweza wa kila kitu***))[33]

### *Muzdalifah*

*Muzdalifah* ni mahali ambako Mahujaji wanafikia baada ya kutoka *'Arafah*, huingia hapo Magharibi na huswali kwa kujumuisha Swalah mbili za Maghrib na 'Ishaa. Hupumzika na kukesha usiku wake hadi asubuhi wanapokwenda kutekeleza taratibu nyinginezo zilizobakia; *Muzdalifah* ni bonde takatifu na hapo wanapaswa Mahujaji kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa wingi kama Anavyoamrisha[34].

### *Jamaraat* na Kuchinja

*Jamaraat* ni mahali pa kurushwa vijiwe kwa ajili ya kufuata Sunnah ya baba yetu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام), pale alipokuwa akimrushia vijiwe shaytwaan kumfukuza, alipokuwa akija kumshawishi asimchinje mwanawe baada ya kuota kuwa kapewa amri hiyo. Shaytwaan huyo alimfuata sehemu tatu na kila sehemu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alimfukuzilia mbali kwa kumpiga vijiwe. Sehemu hizo ni *Jamrat Al-Kubra, Al-Wuswtwaa* na *Asw-Swughraa.*

Kisa chake kinaanza pale Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alipokwenda Makkah kumzuru mkewe na mwanawe, baada ya kuoteshwa amchinje mwanawe Ismaa'iyl (عليه السلام). Alipomuelezea mwanawe kuhudu ndoto yake, mwanawe alikubali kutii amri hiyo. Alimlaza mwanawe kifudifudi ili asiuone uso wake na ili asije kumhurumia akashindwa kutekeleza amri hiyo. Ismaa'iyl (عليه السلام) akasalimu amri na Ibraahiym (عليه السلام) akijitayarisha kumchinja mwanawe. Hapo Allaah (سبحانه وتعالى) Akamfunulia Wahyi Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kuwa asimchinje mwanawe na badala yake akamkomboa kwa kondoo. Maelezo yamekuja katika Qur-aan:

---

[33] At-Tirmidhiy na ameisahihisha Al-Albaaniy katika *Swahiyh At-Tirmidhiy* 3585.
[34] Al-Baqarah (2: 198-199).

﴿ فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ ٱلسَّعۡيَ قَالَ يَٰبُنَيَّ إِنِّيٓ أَرَىٰ فِي ٱلۡمَنَامِ أَنِّيٓ أَذۡبَحُكَ فَٱنظُرۡ مَاذَا تَرَىٰۚ قَالَ يَٰٓأَبَتِ ٱفۡعَلۡ مَا تُؤۡمَرُۖ سَتَجِدُنِيٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٠٢ فَلَمَّآ أَسۡلَمَا وَتَلَّهُۥ لِلۡجَبِينِ ١٠٣ وَنَٰدَيۡنَٰهُ أَن يَٰٓإِبۡرَٰهِيمُ ١٠٤ قَدۡ صَدَّقۡتَ ٱلرُّءۡيَآۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجۡزِي ٱلۡمُحۡسِنِينَ ١٠٥ إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ ٱلۡبَلَٰٓؤُاْ ٱلۡمُبِينُ ١٠٦ وَفَدَيۡنَٰهُ بِذِبۡحٍ عَظِيمٖ ١٠٧ ﴾

**((Alipofikia (makamo ya) kwenda na kurudi pamoja naye; akasema: "Ee mwanangu! Hakika mimi nimeona ndoto usingizini kwamba mimi nakuchinja, basi tazama unaonaje?" (Ismaa'iyl) Akasema: "Ee baba yangu! Fanya yale uliyoamrishwa, utanikuta In Shaa Allaah miongoni mwa wanaosubiri." Basi wote wawili walipojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji (ili amchinje) Tukamwita: "Ee Ibraahiym! Umekwisha sadikisha ndoto! Hakika Sisi hivyo ndivyo Tunavyowalipa watendao ihsaan. Hakika hii bila shaka ni jaribio bayana". Na Tukamfidia kwa dhabihu adhimu))**[35]

**Hajj**

Hajj Maana yake kilugha: Kukusudia

Maana yake kishariy'ah: Kukusudia kwenda *Baytul-Haraam* Makkah kwa ajili ya kutekeleza taratibu za 'ibaadah makhsusi katika kipindi makhsusi.

Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) na mwanawe Ismaa'iyl (عليه السلام) walipomaliza kujenga *Al-Ka'bah* wakaomba Du'aa:

﴿ وَإِذۡ يَرۡفَعُ إِبۡرَٰهِـۧمُ ٱلۡقَوَاعِدَ مِنَ ٱلۡبَيۡتِ وَإِسۡمَٰعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ١٢٧ رَبَّنَا وَٱجۡعَلۡنَا مُسۡلِمَيۡنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةٗ مُّسۡلِمَةٗ لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبۡ عَلَيۡنَآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ١٢٨ رَبَّنَا وَٱبۡعَثۡ فِيهِمۡ رَسُولٗا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَيُزَكِّيهِمۡۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ١٢٩ ﴾

[35] Asw-Swaffaat (37: 102-107).

**((Na (taja) aliponyanyua Ibraahiym na Ismaa'iyl msingi wa Nyumba (*Al-Ka'bah*): "Rabb wetu, Tutakabalie, hakika Wewe ni *as-Samiy'ul-'Aliym* (Mwenye kusikia yote - Mjuzi wa yote). "Rabb wetu, Tujaalie tuwe wenye kujisalimisha Kwako pamoja na *kizazi chetu* wawe ummah wenye kujisalimisha Kwako na Tuonyeshe taratibu za 'ibaadah zetu na Pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni *at-Tawwaabur-Rahiym* (Mwingi wa kupokea tawbah - Mwenye kurehemu) "Rabb wetu, wapelekee Rasuli miongoni mwao ataewasomea *Aayaat* Zako na ataewafunza Kitabu na Hikmah na atakayewatakasa. Hakika Wewe ni A*l-'Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika - Mwenye hikmah wa yote))**[36]

Kisha Allaah (سبحانه وتعالى) Akaamrisha iwe nyumba ya kutekelezwa 'ibaadah bila kumshirikisha na chochote.

﴿ وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِى شَيْـًٔا وَطَهِّرْ بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿٢٦﴾ ﴾

**((Na (taja) Tulipomwonyesha Ibraahiym mahali pa Nyumba (*Al-Ka'bah* Tukamwambia): kwamba: "Usinishirikishe na chochote; na twaharisha Nyumba Yangu kwa wafanyao *Twawaaf*, na wanaosimama (kuswali) na wanaorukuu (na) kusujudu.))**[37]

Kisha Allaah (سبحانه وتعالى) Akamuamrisha Nabiy Ibraahiym (عليه السلام)

﴿ وَأَذِّن فِى ٱلنَّاسِ بِٱلْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾ ﴾

**((Na tangaza kwa watu Hajj; watakufikia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda, watakuja kutoka katika kila njia pana za milima zilioko mbali kabisa))**[38]

Alipoamrishwa hivyo, Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) alisema: "**Ee Mola wangu nitawatangaziaje watu na hali sauti yangu haitaweza kuwafikia watu wote?"** Allaah (سبحانه وتعالى) Akamjibu: "Wewe tangaza kisha ni juu Yetu

[36] Al-Baqarah (2: 127-129).
[37] Al-Hajj (22: 26).
[38] Al-Hajj (22: 27).

kufikisha". Akasimama mahali panapojulikana *'Maqaam Ibraahiym'* na kauli nyingine inasemekana kuwa alisimama juu ya jabali la *Asw-Swafaa* au jabali la Abu Qubays, (Allaah Anajua zaidi) akaita: **"Enyi watu! Mola wenu Ameifanya Nyumba (*Al-Ka'bah* kuwa nyumba ya 'Ibaadah) basi njooni muhiji".** Inasemekana kwamba milima yote ilijiinamisha ili sauti yake ifikie sehemu zote za dunia (na wakazi wake) hata ikawafikia walioko matumboni au ambao hawakuzaliwa bado. Akaitikiwa na kila kilichosikia sauti yake miongoni mwa miji, mawe, miti na kila kiumbe ambacho Allaah (سبحانه وتعالى) Ameandika (katika *Lawh Al-Mahfuwdhw*), majaaliwa ya kutekeleza Hajj mpaka Siku ya Qiyaamah. Na vyote vikaitikia kwa kusema: "*Labbayka Alllaahumma Labbayka*".[39]

'Ibaadah hiyo ikaendelea kutekelezwa na Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) kila mwaka alipokwenda Makkah na baada ya kifo chake ikaendelezwa na mwanawe Nabiy Ismaa'iyl na kuendelea kizazi hadi kizazi.

Lakini 'Ibaadah ya masanamu ikakithiri Bara Arabu na 'Ibaadah ya Hajj ikaingizwa upotofu ndani yake kwa kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) ikawa inatekelezwa kwa itikadi potofu na ma'asi. Masanamu yakatundikwa katika *Al-Ka'bah*, kuta zikajaa mashairi na picha za viumbe zikatundikwa kwenye *Al-Ka'bah*. Maovu yalikithiri hadi kwamba wanawake walitufu *Al-Ka'bah* wakiwa uchi kama walivyozaliwa wakiitakidi kwamba wanapaswa kumkabili Allaah (سبحانه وتعالى). Machafu ya kila aina yalitendwa wakati wa Hajj, kunywa pombe, kuimba, dansi za wanawake n.k. Mashindano ya kila aina ya uovu; kamari, nyimbo, mashairi yalikuwa na nafasi kubwa wakati huo wa Hajj. Pia walishindana kuhusu nani mbora wa ukarimu wa kuwahudumia Mahujaji mpaka akawa anachaguliwa mkuu wa kabila kwa ukarimu wake wa kugawa chakula na maji. K*affaarah* zao za kuchinja zilikuwa za kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kuimwaga damu katika kuta za *Al-Ka'bah* na kutundika nyama katika nguzo zake wakiitakidi kuwa Allaah (سبحانه وتعالى) Amekusudia kutaka nyama na damu za wanyama.

Kutufu kwao pia kulikuwa ni kwa kuimba mashairi na kupiga makofi na miruzi. Qur-aan imetaja hali hiyo:

---

[39] Tafsiyr Ibn Kathiyr (3/221) kama ilivyopokelewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas, Mujaahid, 'Ikrimah, Sa'iyd bin Jubayr na wengineo katika Salaf.

﴿ وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِندَ ٱلْبَيْتِ إِلَّا مُكَآءً وَتَصْدِيَةً ﴾

**((Na haikuwa Swalaah zao (makafiri) kwenye Nyumba (*Al-Ka'bah*) isipokuwa ni miruzi na kupiga makofi))[40]**

Hata *Talbiyah* zao ziliongezwa maneno ya kumshirikisha Allaah (سبحانه وتعالى) walikuwa wakisema:

**لبيك لا شريك لك، إلا شريكاً هو لك، تملكه وما ملك**

"Nimekuitikia huna mshirika isipokuwa aliyeidhiniwa Nawe, unammiliki naye ni mwenye kumiliki anavyomiliki!"

Kinyume na *Talbiyah* ya Tawhiyd:

**لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ, لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ, إِنَّ الْحَمْدَ, وَالنِّعْمَةَ, لَكَ وَالْمُلْكَ, لاَ شَرِيكَ لَكَ**

**"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika kuhimidiwa na neema na ufalme ni Vyako Huna mshrika"**

Hivyo ndivyo ilivyokuwa hali ya Hajj kabla kutumilizwa kwa Nabiy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم). Washirikina waliipotosha kabisa 'Ibaadah hii tukufu iliyoanzishwa kwa Tawhiyd ya Allaah (سبحانه وتعالى) na baba yetu Nabiy Ibraahiym (عليه السلام). Hali ikaendelea hivyo hadi Allaah (سبحانه وتعالى) Alipokidhia du'aa ya Nabiy Ibraahiym (عليه السلام) baada ya kujenga *Al-Ka'bah* alipoomba:

﴿ رَبَّنَا وَٱجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَآ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾ رَبَّنَا وَٱبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَـٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾ ﴾

**(("Rabb wetu, Tujaalie tuwe wenye kujisalimisha Kwako pamoja na *kizazi chetu* wawe ummah wenye kujisalimisha Kwako na Tuonyeshe taratibu za 'ibaadah zetu na Pokea tawbah zetu, hakika Wewe ni *at-Tawwaabur-***

---

[40] Al-Anfaal (8: 35).

***Rahiym* (Mwingi wa kupokea tawbah - Mwenye kurehemu. “Rabb wetu, wapelekee Rasuli miongoni mwao ataewasomea *Aayaat* Zako na ataewafunza Kitabu na Hikmah na atakayewatakasa. Hakika Wewe ni *Al-’Aziyzul-Hakiym* (Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika - Mwenye hikmah wa yote))**[41]

Du’aa ikatakabaliwa kwa kutumwa Nabiy Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) na baada ya miaka ya misukosuko ya da’wah yake akaweza kuitakasa Nyumba ya Allaah (سبحانه وتعالى) na shirki ikatoweka. Abu Hurayrah amesimulia kuhusu Hajj yao kabla ya Hijjat*ul-Wadaa’ii*:

"بَعَثَنِي أَبُو بَكْرٍ الصِّدِّيقُ فِي الْحَجَّةِ الَّتِي أَمَّرَهُ عَلَيْهَا رَسُولُ اللَّهِ (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) قَبْلَ حَجَّةِ الْوَدَاعِ, فِي رَهْطٍ, يُؤَذِّنُونَ فِي النَّاسِ يَوْمَ النَّحْرِ: □ يَحُجُّ بَعْدَ الْعَامِ مُشْرِكٌ وَ□ يَطُوفُ بِالْبَيْتِ عُرْيَانٌ"

Alinituma “Abu Bakr katika Hajj ambayo alichaguliwa na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwa Amiri kabla ya *Hajjatul-Wadaa’i*, pamoja na kundi la watu wawatangazie watu Siku ya *Nahr* kwamba: “***Hakuna kuhiji baada ya mwaka huu mshirikiana yeyote wala kufanya Twawaaf katika Nyumba wakiwa uchi***”[42]

Baada ya hapo Tawhiyd ya Allaah (سبحانه وتعالى) ikathibitika katika ‘Ibaadah hii tukufu hadi leo.

---

[41] Al-Baqarah (2: 128: 129).
[42] Muslim.

## Ramani Maeneo ya Hajj

